**MWITO WA KUTOA MAONI KUHUSU MAOMBI YA VIBALI VYA UJENZI NA LESENI KUTOKA EWURA.**

***Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ni taasisi ya udhibiti wa huduma za sekta nne mchanganyiko inayojitegemea, iliyoundwa kwa Sheria ya EWURA Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania. Shughuli kuu za Mamlaka ni pamoja na kudhibiti kiufundi na kiuchumi sekta za Nishati na Maji kwa Tanzania Bara. EWURA ina wajibu wa kudhibiti shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ndogo ya Mafuta na Gesi Asili.***

Sheria ya Mafuta Na. 21 ya mwaka 2015 inaipa nguvu EWURA, kusimamia shughuli za mkondo wa kati na mkondo wa chini wa sekta ya mafuta ya petroli. Kifungu cha 126 (1) cha sheria hiyo kinamtaka mtu yoyote anayetaka kujenga miundombinu ya mafuta kuomba kibali cha ujenzi kutoka EWURA. Aidha, Kifungu cha 131 (1) cha sheria hiyo kinawataka wote wanaojihusisha na sekta tajwa kuwa na leseni iliyotolewa na EWURA.

EWURA imepokea maombi ya vibali vya ujenzi na leseni kutoka kwa waombaji walioorodheshwa hapa chini. Kutokana na kifungu cha 19(4) cha Sheria ya EWURA, Sura ya 414 ya Sheria za Tanzania, taarifa inatolewa kwa umma kwamba, wafuatao wameomba vibali vya ujenzi ili wajenge miundombinu ya mafuta na leseni kwa ajili ya kujihusisha na biashara/shughuli katika mkondo wa kati na chini wa sekta ya mafuta ya petroli.

| S/N | Jina la Mwombaji | Eneo | Jina la Mkurugenzi/Uraia | Aina ya Ombi la Leseni/Kibali cha Ujenzi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Sun King Tanzania Limited, S.L.P 410, Arusha. | Oloirien, Arusha, Arusha | Kota Kojima | Leseni Jumla ya Gesi ya Kupikia (LPG) |
| 2. | Galco Limited, S.L.P 6244, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 119/1-121, Kitalu “C”, Katete, Momba, Songwe. | Yassir Athuman Nassor | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 3. | Njombe Filling Station Company Limited-Dodoma | Kiwanja Na. 9, Kitalu “J”, Mnadani, | James Malika Mwinuka | Leseni ya Kituo cha Mafuta |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Mipango, S.L.P 411, Njombe. | Dodoma. | | |
| 4. | Hemed Jafari Kingazi/Kingazi Filling Station, S.L.P 68, Mlimba. | Kiwanja Na. 3, Kitalu "D", Kamwene, Kilombero, Morogoro. | Hemed Jafari Kingazi | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 5. | Lake Oil Kagondo Petrol Station, S.L.P 5055, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 464, Kitalu "B", Kagondo, Bukoba, Kagera. | Ally Edha Awadh | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta |
| 6. | Kifaru Oil Investment Limited - Highway, S.L.P 1851, Moshi. | Kiwanja Na. Plot No 874, Kitalu Na. "F", Njia Panda, Moshi, Kilimanjaro. | Mamdali Rajabu Msuya | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 7. | Refuelling Solutions (T) Limited - Tunduru Branch, S.L.P 5421, Ruvuma. | Kiwanja Na. 101, Kitalu "A", Majengo, Tunduru, Ruvuma. | Mohsin Bharwani | Leseni Ya Kituo Cha Mafuta |
| 8. | Oryx Energies Tanzania Limited - Singida Service Station, S.L.P 9540, Singida. | Eneo la Majengo, Singida. | Imani Amos Mtafya | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 9. | Afroil Investment Ltd - Kange Service Station, S.L.P 38383, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 339, Kitalu "B", Maweni, Tanga. | Hilmy Mbarak | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 10. | Mwita Chacha Mashauri, S.L.P 1814, Musoma. | Eneo la Issenye, Serengeti, Mara. | Peter Chacha | Leseni ya Kituo cha Mafuta |
| 11. | Herbert Enock Daffa T/A Kb Petrol Station, S.L.P 64, Korogwe. | Kiwanja Na. 1, Kitalu Na. "26BF", Tangasisi, Tanga. | Herbert Enock Daffa | Kibali cha Ujenzi wa Kituo cha Mafuta |
| 12. | Mansoor Industries Ltd (MOIL), S.L.P 80218, Dar es Salaam. | Kiwanja Na. 64-65, Vijibweni, Kigamboni, Dar es Salaam. | Shanif Mansoor Jamal | Leseni ya Jumla ya Mafuta |

**Mtu yeyote au kikundi cha watu wenye pingamizi kwa mwombaji yeyote aliyetajwa hapo juu kwamba asipewe leseni au Kibali cha ujenzi, anatakiwa kuwasilisha pingamizi hilo kwa EWURA ndani ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kupitia anwani tajwa hapa chini.**

**Imetolewa na**
**Mkurugenzi**
**Mkuu,**
**Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji**